JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Anwani ya simu: 'SIASA'
Simu: 2137232
Fax: 2136924

Kivukoni Ilala CBD
1 Mtaa wa Shabaan
Robert P.O. BOX 63010
**11101 DAR ES SALAAM**

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HA. 322/362/11/97

09 Novemba, 2017

Katibu Mkuu
Democratic Party (DP)
S.L.P 63102
**DAR-ES-SALAAM**

Yah: **TAARIFA YA NIA YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA KUFUTA USAJILI WA KUDUMU WA CHAMA CHA DEMOCRATIC PARTY (DP)**

Naomba urejee suala tajwa hapo juu.

Kifungu cha 9(2)(e) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 [RE: 2015] kinataka chama cha siasa kuchagua viongozi wake kwa njia ya kidemokrasia na kwa vipindi maalumu ambavyo huwekwa katika Katiba ya chama husika. Kifungu hicho kinasema ifuatavyo, nanukuu:-

> *"9(2) Without prejudice to subsection (1) of this section no political party shall quality for provisional registration if by its constitution, policies or activities-*
> *e) it does not allow periodic and democratic election of its leadership."*

Katiba yenu Democratic Party, inasema kuwa viongozi watachaguliwa kila baada ya miaka mitano. Mara ya mwisho chama chenu kilifanya uchaguzi wa viongozi wa kitaifa tarehe 26 Mei, 2012, hivyo uchaguzi mwingine ulipaswa kufanyika siyo zaidi ya tarehe 26 Mei, 2017. Tarehe 26 Mei, 2017 mlifanya uchaguzi batili ambao uliandaliwa na kufanyika kinyume na utaratibu na matakwa yaliyopo katika Katiba na Kanuni za chama chenu. Hivyo, kwa barua ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa yenye kumbukumbu namba HA. 322/362/11/61 ya tarehe 03 July, 2017 Msajili wa Vyama vya Siasa alikataa kutambua uchaguzi huo na kuwataka kufanya uchaguzi mwingine kwa kuzingatia Katiba na Kanuni za chama chenu.

Msajili wa Vyama vya Siasa anasikitika kuona kuwa, kupitia barua zenu zifuatazo:-

- Barua yenye kumbukumbu namba DP 19/06 ya tarehe 05 Oktoba, 2017;
- Barua yenye kumbukumbu namba DP 01/02 ya tarehe 03 Oktoba, 2017;
- Barua yenye kumbukumbu namba DP 19/04 ya tarehe 27 Septemba, 2017; na
- Barua yenye kumbukumbu namba DP 24/09 ya tarehe 19 Septemba, 2017

mmekaidi maelekezo yake ya kuwataka muandae Mkutano Mkuu wa chama chenu na kuchagua viongozi wa kitaifa kukidhi matakwa ya Sheria. Hali hii ina maana kuwa, chama